"Haya (Aibu) haiji ila kwa kheri"

Kutoka kwa Imrani bin Huswain -Radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yao- Amesema: Amesema Mjumbe wa Mwenyezi Mungu -Rehema na Amani ziwe juu yake-: "Haya (Aibu) haiji ila kwa kheri". na katika riwaya nyingine: "Haya ni kheri yote" Au alisema: "Haya yote ni kheri".

[Sahihi] [Imepokelewa na Imamu Muslim - Wamekubaliana Bukhaariy na Muslim]

Haya(Aibu) ni sifa iliyoko katika nafsi inayomsukuma mtu kufanya mazuri au yanayopendeza, na kuacha yanayochafua na kuharibu, na ndio maana haiji isipokuwa kwa kheri, na sababu ya kuja kwa hadithi hii nikuwa mtu mmoja alikuwa akimnasihi ndugu yake kuhusu haya, na akimkataza kuhusu haya, Mtume -Rehema na Amani ziwe juu yake- akasema kumwambia maneno haya.

http://sunnah.global/hadeeth/sw/show/3055